



## USTAWISHAJI WA MALISHO BORA YA MIFUGO

### TANGULIZI

Ili mifugo icheuayo, kama ng'ombe, waweze kushamiri vizuri hawana budi kuwa na malisho bora. Sehemu kubwa ya malisho hayo inatokana na maza'o ya shambani, ikiwemo nyasi. Kuna aina mbalimbali za nyasi zinazofaa, chache katika hizo ni "Cenchrus grass, Rhodes grass, Brachiaria grass, Napier/Bana grass, Stargrass, Pannicum grass, Bothriocloa grass" n.k.

Aina za nyasi maarufu zaidi kwa kuvuna kwa kukata ni Napier/bana na Guatemal grass na kwa kuvuna nyasi kavu (hay) ni Cenchrus grass, Rhodes grass Bothriocloa grass, na Brachiaria grass. Wakati nyasi za Pannicum grass, Mtama na Mahindi machanga hufaa zaidi kutumika kama "Silage". Aidha Nyasi hizi Cenchrus grass na Rhodes grass pamoja na masalia ya mazao kama vile mpunga na mahindi matita yake (hay bales) zitaonyeshwa katika maonyesho haya.

### USTAWISHAJI

Zipo njia tatu za ustawishaji wa nyasi zilizotajwa juu nazo ni:-

- a. Matumizi ya mbegu hai (viable seed). Hapa nyasi husika huweza kupandwa kwa kutumia mbegu zake zilizokomaa vizuri. Mbegu humwagwa kwenye shamba lililolimwa na kulainishwa vizuri na inafaa liwe bichi (si kavu ili mbegu

zing'ang'anie ardhini, zisipeperushwe na upepo kiwango cha kilo 12.5 kwa hektari moja au kilo 5 kwa ekari moja kinatoshwa.

- b. Matumizi ya mashina hai yaliyoachanishwa toka mashina mama. Inawezekana kupata kati ya mashina hai mawili au zaidi yanayofaa kupandikizwa. Kama kawaida, upandikizaji hufanywa kwenye shamba lililotayarishwa vizuri na pia inabidi liwe na unyevu sawia. Nyasi hupandikizwa kwa umbali wa sentimita 60 kwa 30 au sentimita 25 kwa 60, pia nafasi yakupandikiza yaweza kupungua au kuongezeka kutegemeana na ukubwa wa eneo na upatikanaji wa mashina hai ya aina ya nyasi inayo pandwa.
- c. Matumizi ya pingili zilizokatwa (cuttings). Kawaida mashina ya napier/bana au Guatemala grass yaliyokomaa vya kutosha, hukatwa katika pingili za sentimita 30-45 au zaidi/pungufu kidogo na kupandikizwa kwenye shamba lililoandaliwa vizuri. Pia hupaandikizwa kwa umbali kama ule ulioelezwa katika (b) juu.

### MATUNZO

Vyote vilivyopandwa vikishastawi vizuri havina budi kutunzwa. Hii ni pamoja na palizi na uwekaji wa mbolea. Magugu yote

lazima yatolewe kwa mkono – kung’olea kama ifanywavyo kwa mpunga, au kutumia jembe hasa kwa mashamba yaliopandwa kwa njia ya (b) na (c) juu.

Ili kurahisisha kazi zaidi, hasa kwa mashamba yaliyomwagwa mbegu, utumiaji wa kiuu magugu 2,4.D hufanywa kwa kiwango cha mililita 700 kwa hektari moja au mililita 280 kwa ekari moja. Wekea mbolea nyasi zako kila mwaka ili kuongeza mavuno na kufanya nyasi zisizeeke haraka. Mbolea inayofaa zaidi niya samadi lakini kama haitatosha waweza kutumia mbolea ya chumvi chumvi kama “urea au S.A kwa kuimwaga shambani kwa kipimo sahihi. Kuhusu mashamba ya wadudu, hususani mchwa na viwavi jeshi, tumia “furadan” au “aldrini/toxadrin” na “sumithion” sawia. Utatumia “furadan” kuua mchwa kwenye sehemu ndogo yapandikizwa nyasi ambapo “toxadrin hutumika kwenye shamba kubwa zaidi

#### UVUNAJI

Njia zitumikazo

Mazao yakishakomaa ipasavyo huvunwa kama ifuatavyo

- ✦ Kukata kwa mkono nyasi mbichi (hay) bana na Guatemala) au kavu (Cenhrus, Rhodes etc)
- ✦ Mifugo husika kulia horini
- ✦ Kuwachunga ng’ombe shambani wale wenyewe.
- ✦ Kukata kwa mashine na kuwapelekea wanyama horini. Kiwango cha uzalishaji

Kwa upande wa nyasi kavu hasa Cenhrus na Rhodes grass huweza kupata mabunda/matita (bales) 550 au tani 8 kwa hektari moja kwa mwaka kwa mazingira ya Morogoro ambapo kuna mvua za vuli na masika (Bi-modai rainfall regime). Kwa mashamba ya nyasi ambayo mbegu inakusudiwa kuvunwa kiwango cha juu ni kg 120 kwa hektari moja kwa mwaka.

Kwa upande wa “Fodder” hasa kutokana na “napier” au “Guatemala grass” waweza kupata tani 60 – 100 kwa hektari moja kwa mwaka. Majani hukatwa kila baada ya wiki 8 – 12 kutegemea na upatikanaji wa maji na mbolea hasa ya samadi.

#### HIFADHI

Njia zifuatazo hutumika kwa hifadhi ya nyasi:-

1. Kulundika nyasi iliyokatwa chini ya banda lililoezekwa kwa matumizi ya baadaye (loose hay).
2. Kuiacha nyasi ikiwa imesimama shambani kwa matumizi ya baadaye (standing hay)
3. Nyasi iliyofungwa katika mabelo/matita (hay bales) na kuwekwa kwenye mabanda kwa matumizi yabaadaye.
4. Kuhifadhi chini ya shimo (silage)

#### MATUMIZI

Mkulima atatumia nyasi iliyotajwa juu kwa kuwalishia mifugo yake. Lakini akiwa na ziada, anaweza kuuza kwa wafugaji wengine kwa bei nzuri tu kwani belo/tita/bunda moja la nyasi

iliyofungwa laweza kumpatia mkulima kati ya shs. 2500/= na shs. 2800/= kutegemeana na ubora wake.

Licha ya kujipatia fedha kutokana na nyasi iliyofungwa mkulima anaweza kujipatia fedha zaidi kutokana na mbegu za nyasi hasa za “Rhodes” ambapo kilo moja huuzwa kwa shs 12,000/=.

#### MATUMIZI MENGINEYO

Ikishaliwa na mifugo na kuwa kinyesi, ni mbolea nzuri sana mashambani.

Endapo sehemu itakuwa haikuliwa, kama ilivyo baada ya mbegu kuvunwa nyasi inafaa sana kwa kuzuia unyevu ardhini (mulch)

Pia nyasi huzuia momomonyoko wa udongo (Soil erosion control)

#### MWISHO

Ni vyema kwa mfugaji wa aina yeyote kuwa na kishamba/shamba la nyasi ili kukidhi mahitaji ya mifugo yake. Kwa ushauri wa kitaalamu kuhusu ustawishaji wa nyasi bora pamoja na upatikanaji wa mbegu bora za malisho, muone au muandikie:-

MENEJA WA SHAMBA, BOX 3029 SUA – MOROGORO

Simu: 023-2601463

Selula: 0744-319180

0763364980

Fax : 023-2604562